# TAARIFA YA UTENDAJI WA SOKO LA BIMA TANZANIA

# 2019-2021



DKT. BAGHAYO SAQWARE
KAMISHNA WA BIMA
MAMLAKA YA USIMAMIZI WA BIMA
TAREHE 7 OKTOBA 2022
DAR ES SALAAM-TANZANIA



**01** UTANGULIZI

**02** TATHMINI YA VIHATARISHI KATIKA SOKO NCHINI

**03** HALI YA UTENDAJI KATIKA SOKO 2019-2021

**04** CHANGAMOTO, MAFANIKIO NA MIPANGO ENDELEVU



# UTANGULIZI

1. HISTORIA YA SOKO LA BIMA
2. MAJUKUMU YA TIRA
3. OFISI ZA TIRA

# HISTORIA YA SOKO LA BIMA

## KABLA YA UHURU

### 1957

**130**

Hadi kufikia mwaka 1957, idadi ya kampuni za bima zilizokuwa zikifanya kazi nchini ilikuwa takribani kampuni 130. hii ilijumuisha kampuni za bima za kigeni kufungua ofisi za uwakala nchini.

### 1961

**104**

Mwaka 1961 idadi hiyo ilipungua hadi kufikia kampuni 104 kutokana na Serikali kufunga baadhi ya wakala ili kudhibiti utoroshaji wa fedha kwenda nje ya nchi.

## BAADA YA UHURU

### 1967

**NIC**

Sheria ya Bima Na. 4 ya mwaka 1967 ambayo ilizuia kampuni yoyote kufanya biashara ya bima isipokuwa Shirika la Bima la Taifa (NIC) na kuhakikisha kwamba sekta ya bima inamilikiwa na kuendeshwa na Umma.

### 1969

**ZIC**

Aidha, hatua hizo pia zilichukuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar mnamo mwaka 1969 kwa kuanzisha Shirika la Bima la Zanzibar (ZIC).

### 1996

**UHURU WA SEKTA YA BIMA**

Sheria ya Bima Na. 18 ya Mwaka 1996 ambayo ilianzisha Idara ya Usimamizi wa Bima (Insurance Supervisory Department) chini ya Wizara ya Fedha.

### 2009

**TIRA**

Katika kuwezesha maendeleo ya sekta ndogo ya bima, mwaka 2009, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilifuta Sheria ya Bima namba 18 ya mwaka 1996 na kutunga Sheria ya Bima Sura ya 394.

### BAADA YA 2009

1. Kanuni za Bima za mwaka 2009;
2. Kanuni za Bima ndogo ndogo za mwaka 2013; Kanuni za Baraza la Rufaa za Bima la mwaka 2013;
3. Kanuni za Msuluhishi wa Migogoro ya Bima za mwaka 2013;
4. Kanuni za benkibima za mwaka 2019

# MAJUKUMU YA TIRA

Shughuli za Mamlaka hufanyika Tanzania Bara na Zanzibar kwa mujibu wa sheria ya Bima. Majukumu ya Mamlaka yameainishwa katika Sheria ya Bima kama ifuatavyo:

- Kusimamia na kukuza soko la bima lililo madhubuti na salama ili kuwalinda wateja wa bima;
- Kusajili wadau wa bima (Kampuni za Bima, Madalali, Wakala na Wakadiriji wa hasara);
- Kukagua Kampuni za Bima, Madalali ,Wakala na Wasajiliwa wengine wa bima;
- Kushughulikia malalamiko ya bima kutoka kwa wakatabima  na jamii kwa jumla;
- Kutoa elimu ya Bima kwa jamii;
- Kuratibu na kusimamia shughuli za Kampuni za bima, Madalali na Wakala; na
- Kuweka viwango katika kutekeleza biashara ya bima ambavyo vitafuatwa na Kampuni za bima, Madalali na Wakala.

# OFISI ZA TIRA

| KANDA YA NYANDA ZA JUU KUSINI | KANDA YA KASKAZINI | KANDA YA ZIWA | KANDA YA MASHARIKI | KANDA YA KATI |
|---|---|---|---|---|
| Mbeya, Njombe, Rukwa, Katavi, Ruvuma, Iringa na Songwe | Arusha, Manyara, Kilimanjaro na Tanga | Mwanza, Mara, Shinyanga, Kigoma, Kagera, Simiyu, Geita | Dar es Salaam, Pwani, Mtwara na Lindi | Dodoma, Tabora, Singida na Morogoro |

**DAR ES SALAAM OFFICE**


**ZANZIBAR OFFICE**

**HEAD OFFICE-DODOMA**



# MCHANGO WA SEKTA YA BIMA KATIKA PATO LA TAIFA

# MCHANGO WA SEKTA YA BIMA KATIKA PATO LA TAIFA KATIKA KIPINDI CHA MIAKA 10 ILIYOPITA
# (KAMPUNI ZA BIMA PEKEE)




| | 2012 | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Premium as % of GDP | 0.66% | 0.65% | 0.67% | 0.66% | 0.61% | 0.54% | 0.53% | 0.58% | 0.56% | 0.58% |

# MCHANGO WA SEKTA YA BIMA KATIKA PATO LA TAIFA

**1.68%**

BIMA ZA UMMA NA KIBIASHARA

Mchango wa sekta ya bima kwenye pato la Taifa unatarajiwa kuimarika kufuatia utekelezaji wa kanuni za benkibima, kuongezeka kwa wigo wa Bima za lazima na hatua nyingine za usimamizi na udhibiti.

KAMPUNI ZA BIMA


**15.9%**

KWENYESEKTA YA FEDHA



# VIHATARISHI KATIKA SOKO

# TATHMINI YA VIHATARISHI KATIKA SOKO NCHINI



# VIHATARISHI VYA NJE (EXTERNAL RISKS)

## MAANA

Hivi ni vihatarishi vinavyotokana na visababishi nje ya Bima na mara nyingi ni vigumu kuvitazamia na kudhibiti.

## UDHIBITI

Mamlaka inaendelea kutekeleza wajibu wa usimamizi kwa uangalifu na kuweka miongozo na kanuni zinazohitajika ili kudhibiti soko la bima kutokana na athari mbaya za vihatarishi vya aina hii visivyoweza kutabirika

# VIHATARISHI VYA SOKO (MARKET RISKS)

## MAANA

Hivi ni vihatarishi vinavyohusiana na mabadiliko katika mienendo ya bei ya soko inayoathiri uwezo wa mapato wa baadaye wa mali au uwekezaji katika sekta ya bima.

## UDHIBITI

Mamlaka inaendelea kufanya kazi kwa karibu na kwa kuzingatia hatua zinazochukuliwa na Benki Kuu ya Tanzania katika kudhibiti hatari zinazo sababishwa na mabadiliko ya thamani ya fedha zakigeni na hatari ya viwango vya riba.

# VIHATARISHI VYA UKWASI (LIQUIDITY RISKS)

## MAANA

Hivi ni vihatarishi ambavyo mali kioevu inayopatikana katika kampuni za bima zilizo kwenye soko hazitoshi kukidhi madai yaliyokubalika ya wateja, pamoja na madeni mengine na uwekezaji wa mali.

## UDHIBITI

Mamlaka inaendelea kufuatilia mwenendo wa ukwasi wa kampuni za bima kwa kuimarisha mifumo ya usimamizi ili kuhakikisha soko la bima wakati wote linakuwa na uwezo wa kushughulikia majanga yoyote yanayoweza kujitokeza katika soko.

# VIHATARISHI VYA KIUTAWALA (GOVERNANCE RISKS)

## MAANA

Hivi ni vihatarishi vinavyohusiana na mwenendo wa bodi, mgongano wa kimaslahi kati ya bodi na menejimenti ya kampuni, ufanisi wa bodi na mamlaka ya bodi ambayo inaweza kusababisha bodi ya kampuni ya bima kushindwa kutekeleza wajibu wake ipasavyo.

## UDHIBITI

- Mamlaka itaendelea kusimamia uzingatiaji wa kanuni za maadili (code of conduct) katika sekta ya bima Tanzania.
- Mamlaka pia itaendelea kufanya kazi na vyombo vilivyopewa mamlaka kama vile Tume ya Ushindani wa Haki kushughulikia masuala yanayoibua mgongano wa kimaslahi.
- Mamlaka itatoa Mwongozo wa kusimamia masuala ya kiutawala katika kampuni za bima Ili kuhakikisha uwepo wa bodi mahiri kwa lengo la kusimamia biashara za kampuni kikamilifu. Aidha Mamlaka pia itaendelea kusisitiza juu ya muundo sahihi wa bodi kupitia mwongozo utakaotolewa.

# VIHATARISHI VYA UDANGANYIFU (FRAUD RISKS)

## MAANA

Hivi ni vihatarishi vinavyohusiana na miamala ya ulaghai katika ufanyaji wa biashara za bima

## UDHIBITI

Mamlaka inaendelea kufanya kazi kwa karibu na vyombo vingine vya serikali vikiwemo Jeshi la Polisi katika kuhakikisha utekelezaji wa sheria na udhibiti wa vitendo vya uhalifu na udanganyifu.

# VIHATARISHI VYA KIBIMA (INSURANCE RISKS)

## MAANA

Vihatari vinavyohusisha kiwango cha hatari inayopokelewa na kampuni ya bima kulingana na kiwango chake cha mtaji.

## UDHIBITI

Mamlaka inaendelea kufuatilia mwenendo wa kampuni za bima na kuimarisha mifumo ya usimamizi kuhakikisha kampuni zinakuwa na mitaji toshelevu. Pia Mamlaka inaandaa mfumo wa kupima kiwango hitajika cha mtaji wa kampuni ya bima kwa kuzingatia kiwango cha hatari kinachopokelewa na kampuni husika

# VIHATARISHI VYA MATEKELEZO (COMPLIANCE RISKS)

## MAANA

Vinahusisha wasajiliwai katika soko kutokutii sheria, miongozo, kanuni au nyaraka za kiusimamizi zinazotolewa na Mamlaka

## UDHIBITI

Mamlaka inaendelea kusimamia na kufuatilia kwa ukaribu uzingatiaji wa sharia kwa kufanya ukaguzi wa mwenendo wa soko, kutoa maagizo, miongozo na waraka mbalimbali.

# VIHATARISHI VYA KIMTANDAO (CYBER RISKS)

## MAANA

Hivi ni vihatarishi vinavyohusishwa na ukiukaji wa usalama kwa mifumo, taarifa na takwimu zilizomo katika mifumo, na kusababisha tishio kwa uendelevu wa biashara.

## UDHIBITI

Mamlaka ilitoa waraka kuhusu usimamizi sahihi wa usalama wa takwimu na taarifa za mbalimbali za biashara na miongoni mwa hatua nyingine nyingi, kuhakikisha vituo vya msingi vya takwimu katika kampuni zaote za bima vipo ndani ya nchi.

Mamlaka pia inaendelea kutoa msisitizo kwa kampuni na wadau wengine wa bima kuchukua hatua kuhakikisha usalama wa kimtandao ili kulinda ustahimilivu wa soko.



# HALI ILIVYO KATIKA SOKO LA BIMA

# USAJILI MPAKA KUFIKIA SEPTEMBA 2022

WASHAURI NA MADALALI WA BIMA MTAWANYO

4

KAMPUNI ZA BIMA MTAWANYO

3

WAKALA WA BIMA

910

KAMPUNI ZA TAKWIMU BIMA

4

KAMPUNI ZA BIMA

32

WASHAURI NA MADALALI WA BIMA

112

BENKIWAKALA WA BIMA

27

WAKADIRIAJI HASARA

52


# JEDWALI NO 2: USAJILI WA KAMPUNI KIKANDA

| Kanda | Mawakala wa Bima | Benkiwakala | Wataalamu wa Bima | Vituo Vya Uuzaji Bima | Matawi ya Kampuni za Bima |
|---|---|---|---|---|---|
| Kanda ya Ziwa | 105 | 47 | 5 | 10 | 26 |
| | 10.1% | 23.0% | 4.8% | 0.6% | 1.8% |
| Kanda ya Kaskazini | 134 | 38 | 6 | 7 | 31 |
| | 12.9% | 18.6% | 5.8% | 0.4% | 2.2% |
| Kanda ya Nyanda za Juu Kusini | 119 | 14 | 1 | 3 | 16 |
| | 11.5% | 6.9% | 1.0% | 0.2% | 1.1% |
| Kanda ya Mashariki | 594 | 43 | 88 | 1,617 | 1,312 |
| | 57.3% | 21.1% | 84.6% | 97.9% | 93.0% |
| Kanda ya Kati | 32 | 55 | 1 | 4 | 22 |
| | 3.1% | 27.0% | 1.0% | 0.2% | 1.6% |
| Ofisi ya Zanzibar | 53 | 7 | 3 | 10 | 3 |
| | 5.1% | 3.4% | 2.9% | 0.6% | 0.2% |
| Jumla | 1,037 | 204 | 104 | 1,651 | 1410 |

# MAUZO KATIKA SEKTA YA BIMA

Ongezeko la wastani kwa kipindi cha miaka mitano

| | Ongezeko | 2017 | 2021 |
|---|---|---|---|
| Bima za kawaida na Bima za Maisha | 6.9% | 637B | 912B |
| Bima za kawaida | 5.3% | 556B | 746B |
| Bima za Maisha | 17.5% | 80.8B | 165B |



# SABABU ZA UKUAJI KATIKA SOKO



- kuongezeka kwa idadi ya watu wa kipato cha kati ambao huongeza mahitaji ya bidhaa za bima;

- utoaji wa elimu, ubunifu wa njia mpya za usambazaji wa bima ikiwa ni pamoja na teknolojia ya utoaji bima kupitia simu za viganjani kwa lengo la kuwajumuisha wananchi wengi katika soko la bima;

- jitihada endelevu za Serikali katika kuendeleza sekta ndogo ya bima na utulivu wa kisiasa unaoweka mazingira mazuri kwa wawekezaji.

## JEDWALI NA. 3 MWENENDO WA MAUZO YA BIMA KATIKA KIPINDI CHA MIAKA MITANO ILIYOPITA - TSHS MILIONI

| Maelezo | 2021 | 2020 | 2019 | 2018 | 2017 |
|---|---|---|---|---|---|
| Ada za bima za kawaida | 746,446 | 688,643 | 694,894 | 587,631 | 556,298 |
| Ada za bima za maisha | 165,045 | 135,706 | 119,607 | 104,272 | 80,843 |
| Jumla ya ada za bima | 911,490 | 824,349 | 814,501 | 691,902 | 637,141 |

# MAUZO YA BIMA ZA KAWAIDA

Mwaka 2021, mauzo ya Bima za Kawaida yalifikia shilingi bilioni 746.6.

**BIMA ZA VYOMBO VYA MOTO**
35.5%

**BIMA ZA MOTO**
21.5%

**BIMA ZA AFYA**
18.4%

**BIMA ZA AJALI**
7%

**BIMA NYINGINE**
5%

# JEDWALI NA. 4: MWENENDO WA BIMA ZA KAWAIDA KWA KIPINDI CHA MIAKA MITANO TSHS MILIONI

| AINA | 2021 | 2020 | 2019 | 2018 | 2017 |
|---|---|---|---|---|---|
| Moto | 160,189 | 147,236 | 143,457 | 114,095 | 106,565 |
| Uhandisi | 27,373 | 31,704 | 54,701 | 26,190 | 24,985 |
| Vyombo vya moto | 264,738 | 227,174 | 223,627 | 203,151 | 189,898 |
| Ajali | 32,311 | 51,152 | 52,233 | 45,019 | 42,847 |
| Maji | 52,481 | 30,940 | 31,684 | 22,860 | 22,570 |
| Anga | 35,298 | 26,261 | 28,917 | 15,850 | 9,395 |
| Afya | 137,165 | 136,206 | 128,596 | 127,850 | 130,307 |
| Mafuta na Gesi | 519 | 2,788 | 4,549 | 8,958 | 4,224 |
| Nyinginezo | 36,371 | 35,182 | 27,130 | 23,658 | 25,506 |
| Jumla | 746,446 | 688,643 | 694,894 | 587,631 | 556,297 |

# MAUZO YA BIMA ZA MAISHA

Mwaka 2021, bima za Maisha zilifikia shilingi bilioni 165.0.

**BIMA ZA VIKUNDI**

**79.58%**

**BIMA ZA WATU BINAFSI**

**20.4%**

**BIMA ZA MAISHA NYINGINE**

**0.02%**

Aidha, mchango wa bima za maisha katika mauzo ya bima ni asilimia **18.1** ikilinganishwa ni asilimia **81.9** kwa bima za kawaida.

# UKUAJI WA MAUZO YA BIMA (BIMA ZA KILIMO)

- Mauzo ya Bima za Kilimo yalikuwa shilingi bilioni 1.3 mwaka 2021 ikiwa ni asilimia 0.17 ya mauzo yote ya bima za kawaida.
- Ongezeko dogo la mchango wa Bima ya kilimo katika mauzo ya Bima ilitokana na sababu kadhaa ikiwemo:
  - **Uwezo mdogo wa wakulima kumudu malipo ya Bima;**
  - **Kutokupatikana kwa taarifa za kutosha za kilimo ili kuandikisha Bima;**
  - **Kukosekana kwa skimu ya Bima ya kilimo;**
  - **Teknolojia ndogo na miundombinu duni kwa ajili ya uendeshaji bora wa Bima ya kilimo.**

# UKUAJI WA MAUZO YA BIMA

- Kwa ujumla mauzo ya Bima katika kipindi cha mwaka 2021 yaliongezeka kwa asilimia 10.2 kutoka shilingi bilioni 824.3 mwaka 2020 hadi shilingi bilioni 912 mwaka 2021.
- Ukuaji wa soko la Bima umechangiwa na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na:
  - Kuongezeka kwa idadi ya watu wa kipato cha kati ambao huongeza mahitaji ya bidhaa za Bima;
  - Utoaji wa elimu ya Bima;
  - Ubunifu wa njia mpya za usambazaji wa Bima;
  - Matumizi ya teknolojia katika utoaji wa huduma za Bima;
  - Jitihada endelevu za Serikali katika kuendeleza sekta ndogo ya Bima; na
  - Utulivu wa kisiasa na mazingira mazuri kwa wawekezaji.

## JEDWALI NA 5: MWENENDO WA UKUAJI WA ADA ZA BIMA KATIKA KIPINDI CHA MIAKA MITANO TSHS MILIONI

| Maelezo | 2021 | 2020 | 2019 | 2018 | 2017 |
|---|---|---|---|---|---|
| Ada za Bima za Kawaida | 746,446 | 688,643 | 694,894 | 587,631 | 556,298 |
| Ukuaji (%) | 8.4% | (0.9%) | 18.3% | 5.6% | (5.0%) |
| Mchango kwa Jumla (%) | 81.9% | 83.5% | 85.3% | 84.9% | 87.3% |
| Ada za Bima za Maisha | 165,045 | 135,706 | 119,607 | 104,272 | 80,843 |
| Ukuaji(%) | 21.6% | 13.5% | 14.7% | 29.0% | 8.9% |
| Mchango kwa Jumla (%) | 18.1% | 16.5% | 14.7% | 15.1% | 12.7% |
| Jumla ya Ada za Bima | 911,490 | 824,349 | 814,501 | 691,902 | 637,141 |
| Ukuaji (%) | 10.6% | 1.2% | 17.7% | 8.6% | (3.5%) |

# VIONGOZI WA SOKO KATIKA SOKO LA BIMA ZA KAWAIDA

Sehemu hii inatoa uchambuzi wa kina wa vigezo muhimu vya utendakazi kwa makampuni ya bima za kawaida ambayo husaidia kwa muhtasari utendaji wa kampuni. Viashiria hivi vya utendaji ni pamoja na vifuatavyo:

i. Faida ya biashara ya bima za kawaida (Underwriting profit)


ii. Mauzo ya Bima za kawaida (Gross Premium Written)

iii. Uwiano wa Kuhifadhi (Retention rate)

iv. Bima mtawanyo iliyopelewa kwa makampuni ya kigeni (Reinsurance ceded to foreign companies)


# VIONGOZI WA SOKO KATIKA SOKO LA BIMA

## Chati 1: Faida: Bima za kawaida (underwriting Profit)




# VIONGOZI WA SOKO KATIKA SOKO LA BIMA

## Chati 2: Mauzo ya Bima za kawaida (GPW)




# VIONGOZI WA SOKO KATIKA SOKO LA BIMA

## Chati 3: Uwiano wa Kuhifadhi (Retention rate)



# VIONGOZI WA SOKO KATIKA SOKO LA BIMA

## Chati 4: Reinsurance ceded to foreign companies



# VIONGOZI WA SOKO KATIKA SOKO LA BIMA ZA MAISHA


Sehemu hii inatoa uchambuzi wa kina wa vigezo muhimu vya utendakazi kwa makampuni ya bima za Maisha ambayo husaidia kwa muhtasari utendaji wa kampuni. Viashiria hivi vya utendaji ni pamoja na vifuatavyo:

i. Mauzo ya Bima za Maisha (Gross Premium Written)

ii. Mapato ya uwekezaji (Investment Income)


# VIONGOZI WA SOKO KATIKA SOKO LA BIMA ZA MAISHA

## Chati 1: Mauzo ya Bima za Maisha (Gross Premium Written)



# VIONGOZI WA SOKO KATIKA SOKO LA BIMA ZA MAISHA

## Chati 2: Mapato ya uwekezaji (Investment Income)



# BIASHARA YA BIMA MTAWANYO KWA KAMPUNI ZILIZOPO NCHINI

- Mwaka 2021, kampuni mpya ya bima mtawanyo  ijulikanayo kwa jina la Grand Reinsurance Tanzania Company Limited (GrandRe) ilisajiliwa. Hivyo hadi kufikia mwisho wa mwaka 2021 kulikuwa na kampuni mbili za bima mtaanyo ikiwa ni pamoja na Tanzania Reinsurance Company Limited (TanRe).
- Kampuni  hizo mbili za bima mtawanyo ziliripoti ada za bima za ya jumla ya shilingi bilioni 166.0 kwa mwaka 2021 ikiwa ni ongezeko la asilimia 18 kutoka shilingi bilioni 140.6 zilizoripotiwa mwaka 2020.
- Katika mwaka wa 2021, TanRe ilichangia takriban asilimia 99.7 ya ada zote zilivyoripotiwa sokoni na kampuni zote mbili.

# UWIANO WA UHIFADHI (RETENTION RATIO) NA MATUMIZI YA BIMA MTAWANYO

01 **BUMACO** 88.1%

02 **MILEMBE** 85.5%

03 **ASSEMBLE** 83.6%

04 **IGT** 83.6%

**UWIANO WA SOKO**


**52.8%**



# MCHANGANUO WA MAUZO YA BIMA KUTOKANA NA WATOA HUDUMA ZA BIMA

- Mauzo ya bima kwa kipindi cha mwaka 2021 ambapo jumla ya shilingi bilioni 911.5 zilikusanywa kama ada za bima yalijumuisha mauzo kutoka kwa wasajiliwa mbalimbali wa bima kama ifuatavyo:
  - Jumla ya shilingi bilioni 339.6 ya ada za bima ambayo ni asilimia 37.3 ya mauzo yote ya bima, zilipatikana kwa kupitia madalali wa bima.
  - Shilingi bilioni 127.4 ya ada za bima ambayo ni asilimia 14.0 ya mauzo yote ya bima zilipitia kwa mawakala wa bima.
  - Vilevile jumla ya shilingi bilioni 179.1 ya ada za bima ambayo ni sawa na asilimia 19.6 ya ada zote za bima zilizoandikishwa zilipitia kwa benkibima.
  - Kiasi kilichobaki cha shilingi bilioni 265.4 sawa na asilimia 29.1 ya jumla ya ada zote za bima zilizoandikishwa zilipita moja kwa moja kwa kampuni za bima.

# MAUZO YA BIMA KUTOKANA NA WATOA HUDUMA MBALIMBALI



# MAUZO YA BIMA ZA KAWAIDA KUPITIA MADALALI WA BIMA

Katika mwaka 2021, jumla ya TZS 285.1 bilioni za ada ya bima za kawaida zililipwa kupitia madalali, na kuwa na upungufu wa 10.4% ikilinganishwa na TZS 318.2 bilioni ya mwaka 2020. Biashara iliyofanywa kupitia mawakala mwaka 2019 ilikuwa TZS 313.0 bilioni.

Kwa msingi wa aina za bima (Class by class), kiwango cha ushiriki wa madalali katika uandishi wa bima za kawaida hutofautiana kutoka aina moja hadi jingine. Ushiriki mkubwa zaidi wa madalali wa bima ulizingatiwa katika biashara ya Bima ndogo (Micro Insurance) ambapo 100% ya kiasi chote cha malipo kutoka kwa aina hili kilitolewa kupitia madalali wa bima. Hii ilifuatiwa na *general class of business 88.1%,* Moto (49.2%), Uhandisi (47.2%), Marine (46.2%), Ajali (31.0%), Magari (30.9%), Usafiri wa Anga (27.9%). na Afya (27.8%).

# MAUZO YA BIMA ZA KAWAIDA KUPITIA MADALALI WA BIMA-AINA ZA BIMA

| | FIRE | ENGINEERING | MOTOR | ACCIDENT | MARINE | AVIATION | HEALTH | OIL & GAS | MICRO-INSURANCE | OTHER GENERAL |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| NUMBER OF BROKERS | 56 | 32 | 68 | 29 | 24 | 11 | 30 | 0 | 3 | 49 |
| ASILIMIA | 76.7% | 43.5% | 93.2% | 39.7% | 32.9% | 15.1% | 41.1% | 0% | 4.1% | 67.1% |

# MAUZO YA BIMA ZA KAWAIDA KUPITIA MADALALI WA BIMA

Katika mwaka wa 2021, sehemu kubwa zaidi ya biashara ya bima ya kawaida ilishikiliwa na African Risk & Insurance Services (T) Ltd 19.2% (2020: 18.6%), J.H. Minet & Co. (Tanzania) Limited 14.0% (2020: 10.7%), MIC Global Risks (T) Ltd 10.8% (2020: 13.9%), Demeter Financial & Insurance Services Ltd 6.9% (2020: 3.3%), Howden Puri Insurance Brokers Ltd 6.2% (2020: 3.4%) na Impex Insurance Brokers Ltd 6.2% (2020: 5.1%).

Madalali hawa 6 walichangia takriban 63.0% (2020: 55.0%) ya biashara nzima ya udalali wa bima ya kawaida, huku waliosalia wakifanya 37.0% (2020: 45.0%).

# MAUZO YA BIMA ZA NDOGO KUPITIA MADALALI WA BIMA (MICRO INSURANCE)

Ushiriki wa madalali wa bima ulizingatiwa katika biashara ya Bima ndogo (Micro Insurance) ambapo 100% ya kiasi chote cha malipo kutoka kwa aina hili kilitolewa kupitia madalali wa bima. Katika mwaka 2021, jumla ya TZS 2.9 bilioni za ada ya bima ndogo (Micro Insurance) zililipwa kupitia madalali.

| S/n | JINA LA WAKALA | KIASI CHA ADA | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| 1 | TAN MANAGEMENT | 39 | 1% |
| 2 | ACCLAVIA INSURANCE BROKER | 137.1 | 5% |
| 3 | MILVIK TANZANIA LTD | 2,713.3 | 94% |
| JUMLA | | 2,889.4 | 100% |

# MAUZO YA BIMA ZA MAISHA KUPITIA MADALALI WA BIMA

Kufika mwaka 2021, madalali wa bima 16 walifanya biashara ya bima ya maisha (2020: 24). Jumla ya ada ya bima yaliyolipwa na madalali katika biashara ya bima ya maisha yalifikia TZS 54.5 bilioni ikiwa imepungua kwa asilimia 27.4 kutoka TZS 75.1 bilioni mwaka 2020. Katika mwaka 2019 biashara ya bima wa maisha iliyofanywa kupitia madalali ilifikia TZS 60.5 bilioni


**Mchanganuo wa mauzo**

Bima za Maisha za vikundi (Group life)- 41.4%  mwaka  2021 (2020: 67.4%).

Bima za Maisha za kawaida (other life)- 10.6% mwaka 2021 (2020: 12.5%).

Bima za watu binafsi (Individual life) 0.2% mwaka 2021 (2020: 0.3%).

# MAUZO YA BIMA ZA MAISHA KUPITIA MADALALI WA BIMA



# MAUZO YA BIMA KIKANDA

Uandikishwaji wa biashara ya bima na thamani ya ada iliyokusanywa uligawanywa kikanda na kimkoa ambapo kwa mwaka 2021 kanda ya mashariki iliongoza kwa kuwa na kiasi kikubwa cha mauzo ya bima.

- Jumla ya shilingi bilioni 765.8 ambayo ni sawa na asilimia 84.0 ya mauzo yote ya bima ambapo sehemu kubwa ni kutoka mkoa wa Dar es Salaam.
- Kanda hiyo ilifuatiwa na kanda ya kaskazini asilimia 5.6, kanda ya ziwa asilimia 4.3, kanda ya kati na kanda ya nyanda za juu kusini asilimia 1.7, kanda ya Kusini asilimia 0.3 na kanda ya magharibi asilimia 0.2.
- Aidha, kwa upande wa Zanzibar mauzo ya bima yalikuwa asilimia 2.3 ya mauzo yote ya bima nchini.


# JEDWALI NA. 6 MGAWANYO WA MAUZO YA BIMA KIKANDA TSHS MILIONI

| Kanda | Bima za Maisha (A) | Bima za Kawaida (B) | Jumla (A+B) | % ya Mchango |
|---|---|---|---|---|
| Kanda ya Mashariki | 151,185 | 614,593 | 765,778 | 84.0% |
| Kanda ya Kaskazini | 1,728 | 48,905 | 50,633 | 5.6% |
| Kanda ya Ziwa | 2,680 | 36,141 | 38,821 | 4.3% |
| Kanda ya Kati | 421 | 15,420 | 15,841 | 1.7% |
| Nyanda za juu kusini | 864 | 14,549 | 15,413 | 1.7% |
| Kanda ya kusini | - | 2,341 | 2,341 | 0.3% |
| Kanda ya magharibi | 63 | 1,665 | 1,728 | 0.2% |
| Zanzibar | 8,103 | 12,830 | 20,933 | 2.3% |
| Jumla | **135,706** | **688,642** | **911,488** | **100%** |

# MALI NA UWEKEZAJI WA KAMPUNI ZA BIMA

- Mali za kampuni za Bima ziliongezeka kwa wastani wa asilimia 10.1 kwa mwaka katika kipindi cha miaka mitano hadi kufikia shilingi bilioni 1,278.6 mwaka 2021 kutoka shilingi bilioni 862.6 mwaka 2017.
- Madeni ya kampuni za Bima yaliongezeka kwa wastani wa asilimia 8.5 kwa mwaka katika kipindi cha miaka mitano hadi kufikia shilingi bilioni 862.5 mwaka 2021 kutoka shilingi bilioni 586.5 mwaka 2017.
- Uwekezaji wa kampuni za Bima uliongezeka kwa wastani wa asilimia 12.7 kutoka shilingi bilioni 577.6 mwaka 2017 hadi shilingi bilioni 939.7 mwaka 2021.
- Sehemu kubwa ya uwekezaji wa kampuni za Bima kwa mwaka 2021 ulijumuisha Amana katika Benki (42.5%), ikifuatiwa na Dhamana za Serikali (34.0%), uwekezaji katika mali zisizo hamishika (10.7%), hisa (9.9%) na uwekezaji katika maeneo mengine (3.0%).
- Mapato ya uwekezaji yaliongezeka kwa asilimia 3.3 kutoka shilingi bilioni 52.6 mwaka 2020 hadi bilioni 54.3 mwaka 2021.

# MGAWANYO WA UWEKEZAJI MWAKA 2021



# JEDWALI NA. 7: MALI NA MADENI KATIKA KAMPUNI ZA BIMA TSHS MILLIONI

| MALI NA MADENI (TSHS MILIONI) | 2021 | 2020 | 2019 | 2018 | 2017 |
|---|---|---|---|---|---|
| Jumla ya Mali | 1,278,551 | 1,179,470 | 1,047,040 | 936,027 | 862,618 |
| Ukuaji wa Mali (%) | 8.4% | 12.6% | 17.7% | 8.5% | 3.3% |
| Jumla ya Madeni | 862,544 | 780,607 | 719,801 | 655,185 | 586,480 |
| Ukuaji wa Madeni (%) | 10.5% | 8.5% | 9.87% | 11.7% | 3.4% |
| Ziada ya Mali | 416,008 | 399,047 | 327,240 | 280,911 | 276,138 |
| Ukuaji (%) | 7.8% | 16.1% | 16.49% | 12.1% | 3.0% |
| Uwekezaji | 939,694 | 871,727 | 750,828 | 647,294 | 577,593 |
| Ukuaji wa Uwekezaji (%) | 7.8% | 16.1% | 16.0% | 12.1% | 12.5% |

# ULIPAJI WA MADAI YA BIMA

- Moja ya jukumu la msingi la kampuni ya bima ni ulipaji wa madai kwa wateja waliopata majanga mbalimbali.
- Malipo ya madai ya bima za kawaida yaliogezeka kwa asilimia 12.8 kutoka shilingi bilioni 267.5 mwaka 2020 hadi shilingi bilioni 301.9 mwaka 2021.
- Malipo ya madai na mafao ya bima za maisha yaliogezeka kwa asilimia 39.5 kutoka bilioni 68.6 mwaka 2020 hadi bilioni 95.7 mwaka 2021, ongezeko hili kubwa lilitokana na ulipwaji mafao yaliyotokana na vifo katika kipindi cha UVIKO – 19.

# MATUMIZI YA HUDUMA ZA BIMA

- Uwiano wa ada za bima ikilinganishwa na idadi ya watu nchini uliongezeka kutoka shilingi 14,746.8 kipindi cha mwaka 2020 hadi kufikia shilingi 15,334.1 mwaka 2021.
- Ongezeko hili lilitokana na uhamasishaji wa utumiaji wa huduma za bima kwa wananchi.
- Hadi kufikia June 2022, jumla ya Watanzania wanaotumia huduma za bima nchini walifikia 7,829,619 ukilinganisha na watumiaji 6,003,239 June 2021. Ongezeko hili linatokana na uhamasishaji na utoaji elimu ya bima kwa Umma.

# WAAJIRIWA KATIKA SEKTA YA BIMA

- Sekta ya bima imeajiri watumishi wa kudumu 4,158 kufikia Septemba 2022.
- Aidha kwa mwaka 2020 Sekta ya bima ilikuwa na wafanyakazi wa kudumu 3,208.
- Jedwali Namba 8 linaainisha zaidi.

# JEDWALI NA. 8: WAAJIRIWA KATIKA SOKO LA BIMA

| MSAJILIWA | June 2022 | | | June 2020 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | IDADI YA MAKAMPUNI | WASTANI WA WATUMISHI | JUMLA | IDADI YA MAKAMPUNI | WASTANI WA WATUMISHI | JUMLA |
| Wataalamu wa ushauri wa Bima Mtawanyo | 4 | 4 | 16 | 4 | 4 | 16 |
| Wakadiriaji hasara | 52 | 2 | 104 | 60 | 2 | 120 |
| Benkiwakala wa bima | 27 | 25 | 675 | 24 | 13 | 312 |
| Kampuni za Takwimubima | 4 | 4 | 16 | 3 | 4 | 12 |
| Wauza Bima Kidijitali | 4 | 3 | 12 | | 3 | - |
| Wachunguzi Binafsi wa Bima | 3 | 3 | 9 | 3 | 3 | 9 |
| **JUMLA** | **1,127** | **97** | **4,158** | **947** | **80** | **3,208** |

# MAFANIKIO MBALIMBALI KATIKA SOKO LA BIMA

1. **Kodi za Serikali**

- Kampuni za Bima zilichangia kwenye mapato ya Serikali kupitia kodi za mapato ya kampuni kiasi cha shilingi bilioni 15.3 kwa mwaka 2021 ikilinganishwa na shilingi bilioni 14.6 kwa mwaka 2020 ikiwa ni ongezeko la asilimia 4.8. Ongezeko hili lilitokana na kuongezeka kwa faida itokanayo na uwekezaji na hivyo kampuni nyingi kupata faida na kulipa kodi kwa serikali. Vyanzo vingine vya mapato vinajumuisha kodi ya ongezeko la thamani yaani (VAT), kodi ya zuio na tozo mbalimbali kwa Serikali.

2. **Maboresho Ya Mifumo Ya Kielektroniki**

- Mamlaka kwa kushirikiana na makampuni ya bima imeongeza matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma na uwekaji takwimu. Kwa sasa soko la bima linatumia mfumo wa (TIRA Management Infirmation System) TIRAMIS. Mfumo huu umeunganishwa na watumiaji wa huduma za bima nchini. Kwa mfano, ukataji wa bima za magari hauhitaji kutumia stika za karatasi badala yake unatumia mfumo wa kidigitali.

.

# MAFANIKIO MBALIMBALI KATIKA SOKO LA BIMA

### 3. Mapendekezo Ya Mabadiliko Ya Sheria Na Kanuni

- Mamlaka iliandaa mapendekezo mbalimbali kwa ajili ya maboresho ya sheria ya bima, na kanuni za bima ili kuweza kuboresha usimamizi na utendaji wa sekta ndogo ya bima.
- Mapendekezo ya maboresho ya sheria na kanuni yamezingatia ushirikishwaji wa wadau mbalimbali wa sekta ya bima.

### 4. Njia za usambazaji bima

- Jumla ya njia mpya nne (4) za usambazaji wa bidhaa za Bima zimeanzishwa ikiwa ni pamoja na:
  - Benkiwakala wa Bima;
  - Bima ya Takaful;
  - Utoaji Huduma za Bima Kidijitali; na
  - Mfumo wa Maafisa Wauza Bima.

# MAFANIKIO MBALIMBALI KATIKA SOKO LA BIMA

**5**. Kutoa Miongozo ili kuboresha usimamizi wa soko. Miongozo hii inajumuisha:

- Miongozo ya Maafisa Wauza Bima;
- Miongozo ya Takaful;
- Miongozo ya Utoaji Huduma za Bima Kidijitali; na
- Miongozo kuhusu utekelezaji wa viwango vya kimataifa vya taarifa ya kifedha kuhusu mikataba ya Bima (IFRS 17).

## MAFANIKIO MBALIMBALI KATIKA SOKO LA BIMA

6. Kuongezeka kwa wigo wa Bima za lazima ili kujumuisha masoko ya umma, majengo ya biashara, vyombo vya kusafiria majini na uagizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi.

7. Mikakati ya uelimishaji na uhamasishaji kuhusu umuhimu wa Bima iliendelea kutekelezwa ikijumuisha makundi mbalimbali.

# MATARAJIO YA BAADAE

- Kundelea na utekelezaji wa masuala ya Bima yaliyoainishwa katika Mpango Mkuu wa Kuendeleza Sekta ya Fedha ikiwemo, kutekeleza mkakati wa kitaifa wa elimu ya Bima.
- Kutekeleza mkakati wa kitaifa wa Bima jumuishi na kuweka na kutekeleza mfumo madhubuti wa kushughulikia madai, malipo na malalamiko ya wateja.
- Kuanzisha na kutekeleza Mpango wa Kitaifa wa Bima ya Kilimo (National Agriculture Insurance Scheme).

# MATARAJIO YA BAADAE

- Kuendelea kutoa miongozo ya kuboresha usimamizi wa bima ikiwa ni pamoja na:
  - Mwongozo wa uanzishwaji wa muungano wa makampuni kwa ajili ya kutoa huduma za Bima kwenye miradi ya mafuta na gesi (*Oil and gas consortium*);
  - Mwongozo wa taratibu za kushughulikia madai ya Bima;
  - Mwongozo wa utoaji wa huduma za bima kupitia mabenki (Uendeshaji wa Biashara);
  - Mwongozo wa utaratibu wa uwekezaji wa amana ya tahadhari endapo kampuni itaingia katika hali ngumu ya kifedha;
  - Mwongozo wa viwango elekezi vya fidia ya Bima kwa madai ya majeraha ya mwili na vifo kwa mtu wa tatu kutokana na ajali za vyombo vya moto; na
  - Mwongozo wa Utawala Bora kwa Kampuni za Bima.

# CHANGAMOTO MBALIMBALI KATIKA SOKO LA BIMA

- **Kutokuwepo kwa skimu ya Taifa ya Bima ya Kilimo;**
- **Kutokuwepo kwa bodi ya wataalamu wa bima, tawimu bima na hifadhi ya jamii;**
- **Uwezo mdogo wa soko katika kukinga majanga na miradi mikubwa**

# MAPENDEKEZO

**Ili kukabiliana na changamoto za sekta ndogo ya bima zilizoainishwa na kuimarisha mchango wa soko la bima, Mamlaka inawasilisha mapendekezo yafuatayo kwa Serikali**

- Ukamilishaji wa uandaaji wa Sera ya Bima ya Taifa.
- Ushirikiano wa Taasisi na Wizara zinazoguswa na sekta ya kilimo kwa ajili ya uanzishaji wa Skimu ya Taifa ya Bima ya kilimo kwa lengo la kupunguza athari za majanga mbalimbali yanayoikumba sekta ya kilimo kwa Tanzania Bara na Visiwani. Wizara hizo ni Pamoja na Fedha na Mipango, Kilimo, Ufugaji na Uvuvi.

# HITIMISHO

- Kama ilivyo katika Mpango Mkakati wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha (2020/2021 – 2029/2030), mchango wa sekta ya bima kwenye pato la taifa umepangwa kufikia asilimia 3 ifikapo mwaka 2030 na idadi ya watumia kuwa zaidi ya asilimia 50.
- Malengo haya yanahitaji jitihada na juhudi za pamoja ili kufikiwa. Hii ni pamoja na kuboresha mazingira ya uwekezaji kwenye sekta ya bima na kwa wananchi, pia kutumia maendeleo ya kiteknolojia ili kurahisisha utendaji na kufikia watu wengi zaidi hasa ambao wako kwenye sekta ya kilimo, ufugaji, uvuvi na madini.
- Mamlaka ya Bima inashukuru kwa ushirikiano ambao imekua ikipata kutoka kwa Wizara za Fedha na Mipango kwa bara na visiwani pamoja na wadau wote kwenye sekta ya bima.



Asanteni sana